SANAD

# Kujiona Bora Kwa Ajili Ya Imani

## Katika Mizani

Kujiweka kando Uislamu kutokana na washadidivu wanaotumia dini ili kujiona bora kuliko waislamu na wasiokuwa Wai-slamu.

SW

Kwa Jina La (Mwenyezi Mungu) Mrehemevu Mno Mwingi Wa Rehema

*Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah, na rehema na amani zimshukie Bwana wa mitume, na kiongozi wa wanyenyekevu, na juu ya jamaa na maswahaba wake na waliofuata.*

## TABIA NJEMA

Hii dini imekuja kuongoza viumbe wote. Iwalinganie kwenye tabia njema na kuunga ujamaa na kuacha ugomvi na utesi, na kufunza unyenyekevu na ulaini wa tabia, na mengineo katika tabia na maadili bora, hadi Mtume akasema, "Hakika si lingine nimetumilizwa kukamilisha tabia njema."[1] Na akakataza tabia mbaya. Basi akamaliza kwenye hii ardhi: ubaguzi, utabaka, kiburi na kujiona bora. Basi ni ajabu sana kwa ambae anaasisi fahamu ambazo zinapinga yale ambayo amekuja nayo bwana wa Mitume, huku akidai kuwa hili ni katika imani! Na katika fahamu ambazo zinapinagana waziwazi ni "isti'laa (kujiona bora) kwa ajili ya imani".

## LINI ILIASISIWA FAHAMU YA KUJIONA BORA KWA SABABU YA IMANI?

Katika fahamu makosa na upotoshaji mbaya za vikundi shadidivu ni fahamu ya "kujiona bora kwa sababu ya imani."

Aliyeasisi fahamu hii ni mshairi ustadhi Sayid Qutb katika kitabu chake "Fi Dhilal al-Quran" na pia ameitaja kwenye kitabu chake "Ma'alim fi at-Tariq" kwenye makala kwa anwani "Ubora wa Imani"! Na vikundi shadidivu vimechukuwa fahamu hii na kuitumia njia ya kujiona bora ni kujiweka juu hata ya baba zao, mama zao, walimu zao na mashekhe wao, hawachungi haki yoyote ya yeyote kwa ajili ya hilo, bali huenda tukasikia mmoja wao amemuua mamake katika swala baada ya kumkufurisha.

Wala fahamu hii ya "kujiona bora kwa ajili ya imani" hatukuipata kwenye zama za Mtume wala maswahaba wala waliowafuata wao katika karne tatu za kwanza, wala hata karne zilofuata baada ya hapo, si kwa matamshi yake wala kwa maana yake! Bali Uislamu umekuja kinyume chake.

(1) Imepokewa na Ahmad (8952), na Bukhari katika Al-Adab Al-Mufrad (273), na Hakim (2/613) na wengineo kutokamana na hadithi ya Sayyiduna Abu Hurayra --Mungu amridhie-- ameipandisha.

## WASHADIDIVU WAMEFAHAMU VIPI MAANA YA "KUJIONA BORA KWA AJILI YA IMANI"?

Ni kuwa muumini amuangalie kila ambae anatofautiana nae kwa mtazamo wa uduni na kumdharau hali yake, kwani asiekuwa yeye ni mtu wa jahiliya na amepotea!

Anasema katika "Fi Dhilal al-Quran" (1/145): "Na akawapatia ubora ambao kwayo wanaangalia vipote vya wanadamu waliopotea katika pambizo za ujahiliya uliojaa kila kipembe katika ardhi, hapo wanahisi kuwa Allah amewapatia wao ambalo hakuwapatia walimwengu wengine."

Kwahivyo, Ustadhi Sayid Qutb anajenga fahamu ya hatari ambayo tunaweza kuiita "Kiburi cha Kiislamu."

Na hatujui fahamu hio italingana vipi na hisia inayoundika kwenye moyo na hisia ya mtu kwa maneno yake Allah: {Na watasema: Alhamdulillah! Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye aliye tuhidi kufikia haya. Wala hatukuwa wenye kuhidika wenyewe ingeli kuwa Mwenyezi Mungu hakutuhidi} [Al-A'raaf:43]. Na neno lake {Na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni, ijapo kuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea} [Al-Baqara:198].

Na hailingani kuona kuneemeshwa na Allah, na kuhisi fadhila Yake, pamoja na kumdharau mwengine na kujiona bora kwa namna yoyote itakayokuwa au kwa jina lolote litakalokuwa, kwani anaejua upungufu wa dhati kutoka kwenye nafsi yake, na kuwa yale aliyomo ndani yake ni fadhla ya Mola pekee hawezi kujiona bora kwa yule ambae hakupewa alichopewa yeye.

## FIKRA POTEVU... NA MALIPIZO

Hio fikra ya ajabu geni ambayo haina mafungamano yoyote na Uislamu, haiambiwi ispokuwa ya kuwa ni fikra potevu.
Na mwenye fikra hii ndiye anaefaa zaidi kuitwa ni wa jahiliya kuliko yule anaedai kuwa yeye ni bora kumliko!

Kwani sisi tunaiona hii fikra imejaa maana na tabia ambazo zinakhalifu sheria (ya Kiislamu) na mfumo wa Mtume. (Tabia mbaya kama) kujiona bora na kuwadharau wengine, iliyojawa uadui na chuki, na kumkataa mwengine. Tabia hizi si lingine zinaashiria nafsi zenye maradhi zinaugua dhiki na kunyimwa, ambayo yamezaa ambayo tunayaona katika malipizo ya kulingania kuwa na ubora kwa ajili ya imani na mengineo.

Kwani taabu waliyoipata hawa ilikuwa na athari kubwa sana katika nafsi zao na fikra zao na mielekeo yao ya kiadui dhidi ya serikali na jamii, bali na dhidi ya kila anaetofautiana nao.
Wakawa wanatafuta katika nukuu na kuzikata kulingana na muradi wao bila kuzingatia muktadha na misingi.

## NI ZIPI DALILI ZA WENYE KUFUATA FAHAMU HII

Sayyid Qutb ametumia aya kwenye Quran na misimamo miwili ya wema waliopita, kuwa ndizo dalili.
Aya ni: {Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini} [Aal Imran:139].

Na katika misimamo ya wema waliopita, ametaja matukio mawili ya maswahaba (radhi za Allah ziwe juu yao):

**1. Wa kwanza ni msimamo wa Swahaba Mughira bin Shu'ba kwa Rustum, kiongozi wa Fursi.**

**2. Wa pili, ni wa swahaba Rab'i bin Aamir kwa Rustum pia kabla vita vya Qadisiya.**

Na visa hivi viwili vinaonyesha kughurika kwa dunia na mapambo yake, na maswahaba hawa wakakabiliana na hili kwa kujitukuza kwa dini na kutogeukia mapambo haya, na kulingania kutokana na kuabudu waja na kuelekea kumuabudu Mola wa waja (aliyetukuka shani).

Na amefungua maneno yake kwa kuijengea dalili fahamu yake ya makosa kwa kupitia hii aya, “La kwanza linalokuja kwenye akili kutokana na mwelekezo huu ni kuwa inaelekeza kwenye jihadi ambayo inadhihirika kwa vita.” Kisha akatadaraki kwa kusema, “Lakini uhakika wa mwelekezo huu na upeo wake ni mkubwa na mbali zaidi kuliko hali hii moja… kwa kila maingiliano yake mengi.”

Anaieneza hali hii ambayo anaitetea kwa kusema, “Hakika hii inaashiria hali ya daima ambayo inafaa iwe ni hisia ya muumini, fikra yake, kukadiria kwake kwa vitu, matukio, maadili na watu wote. Hakika hii inaashiria hali ya kujiweka juu (kujiona bora), ambayo inafaa ndiyo itulie kwenye nafsi ya muumini mkabala wa kila kitu, kila hali, kila maadili na kila mtu. Kujiona bora kwa ajili ya imani na maadili yake juu ya maadilo yote ambayo hayatokamani na msingi wa imani.”

Na hatujui ustadhi mshairi ametoa wapi hii kuwa {kwani nyinyi ndio wa juu} maana yake ni kujiona bora sababu ya imani??!!

## WANAZUONI WA UMMAH WAMEFAHAMU VIPI MAANA YA AYA HII

### Kwanza, maana ya "isti'laa" katika Qurani:

1. Maana ya kwanza: kushinda: Kama mfano katika aya: {..na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakaye shinda.} [Taha:64] yaani mwenye kushinda. Imefasiriwa hivo kwenye Taj al-Arus ya Zabidi (7/27).

Na aya: {Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini} [Aal Imran:139]. Na: {Basi msiregee na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakao shinda. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi, wala hatakunyimeni malipo ya vitendo vyenu) [Muhammad:35]. Yaani ilhali nyinyi mumeshinda na mumenusurika, na maana iko wazi kulingana na msururu wa aya.

2. Maana ya pili: kufanya kiburi na kujiweka juu.
Nayo ni haswa kwa Allah kama unaposema “Subhanahu wa Ta’ala (aliyetukuka na aliye juu)” yaani amekuwa na kiburi na amejiweka juu kutokana na kila ambalo halilingani na Dhati Yake tukufu.
Nayo kwa maana hii, kwa viumbe ni tabia mbaya iliyokatazwa katika sheria na imepokewa katika hadithi qudsi: “Kiburi ni sifa yangu na utukufu ni sifa yangu, basi atakaeshindana nami katika mojawapo nitamwingiza jahanamu,”[2] na katika mapokezi: “nitamvunja.”
Na Mtume - rehema na amani zimshukie- amesema: “Haingii peponi ambae moyoni mwake atakuwa na mfano wa tembe ya kibri.”[3]

## PILI: MAJIBU YA WENYE KUFASIRI QURANI NA WANAZUONI KWA UPOTOFU WA ALIYEKHALIFU KATIKA KUTUMIA DALILI

Na nukta ya kutofautiana katika mas'ala haya ni kupotoa maana ya {nyinyi ndio wa juu}.
Na imekuja katika aya mbili kwenye Quran, kwenye Suratu Aal Imran aya ya 139 na kwenye Suratu Muhammad aya ya 35.
Na maana ya {nyinyi ndio wa juu} kama walivyosema wafasiri ni washindi, mulionusurika.

Amesema Shekhe wa wafasiri at-Tabari katika tafsiri yake (6/76): {Wala msilegee}, enyi maswahaba wa Muhammad, yaani musidhoofike kwa ajili ya yale yaliyowapata Uhud kutoka kwa adui wenu kutokana na mauwaji na majeraha, musidhoofike katika jihadi dhidi ya adui wenu na kupigana nae {wala msihuzunike}, wala musihisi huzuni mukababaika kwa hakika {kwani nyinyi ndio wa juu} yaani mulioshinda na mulionusuriwa, na nyinyi ndiyo muna mwisho wa ushindi na kunusuriwa dhidi yao {mkiwa ni Waumini}.

2-Imepokewa na Ahmad (7382), na Abu Daud (4090), na ibn Majah (4174) na wengineo kutokamana na hadithi ya Abu Hurayra –Mungu amridhie– ameipandisha.

3- Imepokewa na Muslim (91) [Kitabu cha Imani] na wengine kutokamana na hadithi ya Abdullah bin Mas'ud –Mungu amridhie– ameipandisha.

Na Imam at-Tabari katika kufasiri hivi ameafikiana na maimamu wengi, miongoni mwao ni:

1. *Ad-Dhahhak bin Muzahim (aliyefariki 102) Tafsiri ya Ibn Abi Hatim (3/771)*

2. *Al-Imam Mujahid bin Jabr (aliyefariki 103) Tafsiri ya at-Tabari (21/228)*

3. *Muqatil bin Sulayman (aliyefariki 150) katika tafsiri yake (4/53)*

4. *Abu Ishaq al-Tha'labi (aliyefariki 427) Tafsiri ya Al-Kashf wal-Bayan (3/172)*

5. *Nasir ad-Din al-Baydhawi (aliyefariki 685) Anwar at-Tanzil (5/125)*

6. *Al-Imam an-Nasafi (aliyefariki 710) Madarik at-Tanzil wa Haqa`iq at-Ta`wil (1/295)*

7. *Al-Imam Abu Hayyan al-Andalusi (aliyefariki 745) Al-Bahr al-Muhit (3/353)*

8. *Al-Imam Ibn Kathir (aliyefariki 774)*

Na Imam ar-Razi ametaja maana nyingi za aya, kisha akasema kuhusu hii maana tuloitaja kuwa "ndiyo inayofungamana zaidi na muktadha wa kabla yake" (9/12).

Haya ndiyo maneno ya wafasiri na hakuna ile maana alioileta Sayyid Qutb kwa njia yoyote, kwa karibu au mbali!
Ili ndiyo uone namna ya upotoshaji wa maana ya aya, na ujue makosa ya kuitumia hii aya kama dalili.
Sayyid Qutb alikuwa ni mshairi na hakuwa Msomi wa misingi, na namna ya kutoa maana, ndipo kalamu yake ikamtelezesha kwenye maana hii iliyopotoka, na akawaathiri wafuasi wake na kusababisha kughurika na kuwaingilia wengine.
Akapotoka kutokana na maana ya asili ambayo ni kuwa muislamu hafai kupatwa na udhaifu au unyonge, nayo ndiyo makusudio yao wanaposema, "Haki inakaa juu na haikaliwi juu."
Wakaenda kwenye maana kuwa muislamu au muumini anapaswa ajiweke juu ya viumbe sababu yeye ni muumini, na kuwa asiyekuwa muumini ni jahili mpotevu, inapasa muumini ajiweke juu yake hali ya kuwa na nguvu au udhaifu.

## BAINA YA UTUKUFU NA KIBRI

Katika matukio mawili ambayo aliyekhalifu ameyatumia kama dalili, wale maswahaba wawili walikuwa mbele ya kiongozi wa jeshi la adui akiwa na wafuasi wake na gogi lake, akijaribu kwa kibri chake kuingilia utukufu wa muislamu. Hapo wakadhihirisha utukufu wa uislamu na kuwa wao ni waja wa Allah wenye kuitaka akhera mkabala wa kujifakhiri na ukafiri na kuitaka dunia.

Na hapa kuna kisimamo...

Inachanganya sana baina ya utukufu na heshima ya muislamu na baina ya kiburi na kujiona bora zaidi ya wengine, ambayo Allah ameikataza hata kwa asiyekuwa muislamu.

Na kuhusu hilo Allah amesema: {Hayo ndiyo makaazi ya Akhera, tumewafanyia wale wasio taka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wacha Mungu} [Qasas:83].

Zingatia neno Lake {wasio taka kujitukuza duniani}. Hakuwavua waislamu kwa kujuzu kutaka kujitukuza kwenye ardhi.

Lakini cha ajabu ni kuwa sisi hatuko katika kutopambanua baina utukufu na kiburi, bali ulinganizi hapa uko wazi kutuelekeza kwenye kujiweka juu, kufanya kiburi na kudharau wengine, kama inavyodhihirika waziwazi katika miamala ya wenye kuthibitisha fikra hii.

Wala haifai kusemwa kuwa kiburi kinafaa kwa makafiri na mafasiki, sababu hili hata kwa waliojuzisha wameweka vidhibiti maalumu. Mwanachuoni Al-Qarafi anasema katika kitabu A-Furuq (4/245): "Asili ya kiburi ni haramu. Na huenda ikaizukia ambayo huifanya iwe wajibu kama kuwafanyia kiburi makafiri katika vita na kwengineko..."

Na Mungu hamkuruhusu mtu kufanya kiburi. Na si lingine ni ulinganizi wa iblisi {Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye} (Al-A'raaf:12). Anawadanganyia nao binadamu ili awaangushe kwenye dhambi ambayo imemsababisha yeye afukuzwe.

## MAANA YA NENO LAKE ALLAH {WENYE NGUVU JUU YA MAKAFIRI}

Na huenda wakatumia dalili ya aya: {Enyi mlio amini! Atakaye iacha miongoni mwenu Dini yake, basi Mwenyezi Mungu atakuja leta watu anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigania Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anaye laumu} [al-Ma`ida:54].

Aya hii na aya nyinginezo ambazo zimekuja kwa maana ya kuwafanyia ugumu makafiri zimefungamana na hali ya kupigana vita, na wala sio asili ya waislamu kuamiliana na wengine kwa vizuri, kama ilivyothubutu katika mwenendo wake Mtume (rehema na amani zimshukie) na maswahaba wake watukufu.

Na maana ya aya ni {wanyenyekevu} wenye upole {kwa Waumini na wenye nguvu} wagumu {juu ya makafiri, wanapigania Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anaye laumu}. Imetumiwa harufu ya 'وَ' ya kuonesha hali, yaani wanapigana na makafiri ilhali hali yao ni kinyume na wanafiki, kwani wanafiki walikuwa na urafiki na mayahudi, kwahio wanapotoka katika jeshi la waislamu walikuwa wakiwaogopa marafiki zao katika mayahudi, basi walikuwa [4] hawafanyi jambo ambalo wanajua litawaletea lawama kutoka kwao.

## NAMNA MASWAHABA WALIVOFAHAMU NA KUTEKELEZA UTUKUFU WA UISLAMU

Kuna misimamo mengi ya maswahaba ambayo inabainisha maana inayotakikana na nzuri ya utukufu wa muislamu.

Huyu hapa sayyidna Umar bin al-Khattab (radhi za Allah ziwe juu yake) anatubainishia utekelezaji wa kivitendo wa utukufu na sio kujiweka juu na kujiona bora kwa waislamu na kwa wasio kuwa wao, kama tunavyoona kutoka kwa washadidivu na wakufurishaji...

Sayyidna Umar bin al-Khattab (radhi za Allah ziwe juu yake) alipoenda Shaam na ilhali amevaa kikoi, khufi na kilemba na huku amemshika ngamia wake anaingia nae kwenye maji.

Wakamwambia, “Ewe amirul muminin, majeshi na wakubwa wa Shaam watakutana na wewe ilhali uko kwenye hali hii.” Basi Umar alisema, “Sisi ni watu Mungu ametutukuza kwa uislamu. Basi hatuutafuti utukufu kwa linginelo.” Nao ni msimamo unaodhihirisha maana ya utukufu kwa hii dini na kutoghurika na Shetwani na upotevu wake na kupamba kwake upotevu na ukafiri. Na katika msimamo huu huwezi kuhisi maana yoyote ya utukufu kwa ile maana ambayo wanaileta na kuitangaza na hawa waliosoma na walinganizi wa fikra hii shadidivu.

(4) Tafsiri ya al-Kashshaf (1/643), tafsiri ya al-Jalalayn (1/147).

## HAKUNA KUJIONA BORA KATIKA UHAI WA MTUME, MWISHO WA MANABII

Kisha iko wapi hii kujiona bora kwa ajili ya imani --kama namna wao wanavyoiita-- katika kuamiliana Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) na makafiri wa kiqurayshi katika muda wake wote wa ulinganizi mtukufu ndani ya Makka.

Hata kama baadhi watataja hili kwa kuwa
Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) alikuwa dhaifu ndani ya Makka
Tunasema: Kwanza : hii haileti tafauti kwa huyu aliyekhalifu kwani yeye anasema katika kitabu "Ma'alim Fi at-Tariq": "Kujiona bora... kukiwepo na udhaifu wa nguvu na uchache wa idadi na uchache wa mali ni sawa sawa na kujiona bora kukiwepo nguvu, wingi na utajiri."
Pili, haifai kuwa ni hoja sababu Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) siku ya Fat'hi Makka alikuwa katika hali ya vita na makafiri ambao walimuudhi na walimtoa, na waliadhibu maswahaba zake na walimuua ami yake. Na ameingia Makka ilhali ni mshindi, na pamoja na hivi, alidhihirisha huruma na ulaini kwa makafiri wa kiqurayshi kiasi cha kutoweza ulaini wowote wala huruma yoyote kukurubia kiwango chake...
Kwani alikuwa akiinamisha kichwa chake hadi ndevu zake tukufu zilikuwa zikigusa kipando chake ngamia wake, akaingia hali ya kusujudu mnyenyekevu kwa Mola wake aliyetukuka.
Zingatia maneno yake katika kuamiliana kwake na makafiri hata katika hali ya vita kwenye Fat'hi Makka kwa ajili ya kulea umati wake (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake): "Leo hakuna lawama juu yenu. Mungu awasamehe... Nendeni kwani nyinyi muko huru."
Na anamwambia Uthman bin Talha baada kumrudishia ufunguo wa al-Ka'ba:
"Shika ufunguo wako ewe Uthman. Leo ni siku ya wema na kutekeleza."
Na Saad bin Ubada aliposema, "Leo ni siku ya vita," alisema, "Amesema urongo Saad. Leo ni siku ya huruma."

## MANENO LAINI

Bali Mungu aliyetukuka amewaamrisha manabii waseme maneno laini. Ikawa katika amri yake kwa Nabii Musa na nduguye Harun (amani iwe juu yao) katika kukabiliana na Fir'aun: {Nendeni kwa Firauni. Hakika yeye amepindukia mipaka. Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa. Wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tunaogopa asije akapindukia mipaka juu yetu au kufanya jeuri. Akasema: Msiogope! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na ninaona.} [Taha 43-46]

Na maana ya {Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na ninaona} si ni kama {Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu} Zote mbili ni kwa maana ya kuwapa kuthubutu, nguvu na ushindi na sio kama alivyodai mwenye kukhalifu!

## MFUMO WA QURAN KATIKA KUAMILIANA NA ANAETOFAUTIANA

Katika Sheria tukufu na uongozi wa Mtume mtukufu, hakuna amri au uelekezi kwa maana waliyoifahamu wao. Hakuna kuamrishwa kujiona bora kwa mtu au fikra au kanuni.
Na hakika si lingine, Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) ametuletea kufuata haki na kuinusuru, na kutoghurika na batili. Na ulikuwa uongozi wake katika kuwalingania viumbe ni alivyoteremsha Mola wake kwenye Quran tukufu:
{Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka.} [an-Nahl:125]
{Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa.} [al-Ankabut:46]
{Waambie waja wangu waseme maneno mazuri, maana Shet'ani huchochea ugomvi baina yao. Hakika Shet'ani ni adui aliye dhaahiri kwa mwanaadamu.} [al-Israa:53]
Na ulikuwa katika uongozi wa Allah kwa Mtume wake wakati maadui wanaifanyia inadi haki na wanaghurika na batili:
{Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Wala wasikupaparishe hao wasio kuwa na yakini.} [ar-Rum:60]
{Basi subiri, kama walivyo subiri Mitume wenye stahmala kubwa, wala usiwafanyie haraka.} [al-Ahqaf:35]
{Basi subiri kwa subira njema.} [al-Ma'arij:5]
Na Mungu aliufundisha adabu ummati wake akasema:
{Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!} [al-Furqan:63]
{Hayo ndiyo makaazi ya Akhera, tumewafanyia wale wasiotaka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamungu.} [al-Qasas:83]
{Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.} [Luqman:18]
Hii ndiyo amri ya Mwenyezimngu kwa Mtume na Ummati wake kuwaamrisha namna ya kuamiliana na wenye kukhalifu na kukanusha wapingaji haki, wenye kulingania na kusaidia batili.

Na kila neno la "ujuu" kwenye aya lamaanisha kusubiri na kushikamana na haki na kutoghurika na ukanushaji wa wenye kukanusha na upingaji wa wanaokadhibisha, pamoja na moyo kufangamana na Mola na kuwa na yakini na nusra yake.

Katika yaliyotangulia, yako wapi maneno ya aliyekhalifu aliposema: "Kujiweka juu na kujiona bora... pamoja na udhaifu, uchache wa idadi na ufukara wa mali ni sawa sawa na kujiona bora pamoja na nguvu, wingi na utajiri."

## HIKMA NI KITU ANACHOKITAFUTA MUUMINI

Kuhusiana na fikra, basi Mwenye sheria (Mtume, Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) ametufunza kama alivyofunzwa na Mola wake, nayo ni kuwa kanuni na ada basi kila ambalo litaafikiana na haki katika hilo basi sheria hulikiri na kulikubali hata kama litatoka kwa mtu ambae hathaminiwi na watu. Na ambalo litakhalifiana na haki basi litarudishwa na halikubaliwi kwa njia yoyote itakayokuwa.

Na zingatia neno la Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) kuhusu makubaliano alioushuhudia katika jahiliya:

"Nimeshuhudia makubaliano katika nyumba ya Abdullah bin Jud'an, sipendi kupewa hata ngamia wekundu ili nikhalifu, na lau katika uislamu nitaitwa kwa ajili yake pia nitaitikia."[5]

Na malengo ni kuwa tabia njema zipo katika ubinadamu, zimeenea kwa viumbe, na uislamu umekuja kuzikikiri na kulingania kwazo na kuzitilia mkazo. Basi wakati wowote muislamu atakapokutana nazo basi anazikubali na hazikanushi na anakuwa anazistahiki zaidi.

(5) Sirah ibn Hisham (1/134).

## UFUPISHO

1.Kujiweka juu na kujiona bora sababu ya imani ni katika fahamu za makosa zilozuliwa ambazo zinakuza kiburi na kudharau wengine kwenye nafsi. Aloziasisi ni Sayyid Qutb katika vitabu vyake. Na washadidivu na wakufurishaji wakazifanyia kazi katika miamala yao na waislamu na wasokuwa waislamu kama inavyoshuhudiwa.

2.Fahamu hii ya makosa haina matamshi ya wazi au dalili, ispokuwa maoni na uchambuzi wa mshairi ambae hakuwa na ilimu ya kutosha kama inavyojulikana. Na hatukupata maana au tamshi hili la "kujiona bora kwa ajili ya imani" katika miongozo ya Qurani, Mtume, karne tatu za kwanza na baada yao.

3.Aliyekhalifu ametumia aya na matukio mawili ya maswahaba kuwa ndiyo dalili. Ama aya basi amewakhalifu wenye kufasiri na wenye ilimu na ameenda kwa namna ambayo inakhalifu misingi na makusudio ya dini. Ama hayo matukio mawili basi amechanganya baina utukufu wa muumini na baina ya analolilingania yeye kutokamana na kujiona bora na ujuu.

4.Kuna tofauti baina utukufu ambao anafaa kuwa nao muumini kutokamana na kuwa mja wa Allah na kuitaka akhera mkabala wa kughurika na gogi la ukafiri na kuitaka dunia, ni tofauti na kujiona bora ambayo Sayyid Qutb analingania na wanayotekeleza katika zama zetu waliosoma fikra hii kwa kiburi na madharau.

5.Katika Maisha ya Mtume (Rehema na amani zimshukie) hakukupatikana kujiona bora si pamoja na waislamu wala si pamoja na wasiokuwa wao, si katika vita wala kwingine, na hakika si lingine yaliyoko ni mapenzi, huruma, unyenyekevu na wema.

6.Hii maana ya kujiona bora kwa watu, fikra na kanuni ambayo wanailingania hawa waliokhalifu haipatikani katika sheria tukufu wala uongozi wa Mtume. Na hakika si lingine ni kuwa Mtume (Rehema na amani zimshukie na jamaa zake) amekuja kufunza kufuata haki na kuinusuru na kutoghurika na batili.

DAR AL FAQIH
مؤسسة طابة
Tabah Foundation
www.tabahfoundation.org

www.sanad.network
facebook.com/sanadnetwork
twitter: @sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork